



Beta thalasemia ni ya kawaida sana kwa watu wanaoishi Mashariki ya Kati, Afrika, Asia Kusini (India, Pakistani, n.k.), Asia ya Mashariki-kusini na wazaliwa wa China.

Watu walio na dalili za beta Thalasia kwa kawaida hawataonyesha matatizo yoyote ya kiafya isipokuwa upungufu mdogo wa damu.

Huenda ukawa na dalili za beta Thalasia na usijue.



Cooley's Anemia Foundation
330 Seventh Avenue, Suite 200 New York, NY 10001
(212) 279-8090 FAX (212) 279-5999

www.thalassemia.org

Swahili

Je, Umepimwa
Dalili za Beta
Thalasia?

Thalasemia ni jina la kundi la matatizo ya damu ya jenetiki. Zaidi ya watu milioni mbili nchini Marekani wana dalili za jenetiki za thalasemia.

Huenda ukawa nazo pia.

Kuna sababu mbili muhimu sana za wewe kujua kama una **dalili za beta thalasemia**:

Kwanza, wakati watu wawili ambao wana **dalili za beta thalasemia** wanapata mtoto, kuna uwezekano mmoja kati ya nne (**asilimia 25**) kuwa **kila** ujauzito ambao mtoto atazaliwa utakuwa na **matatizo makubwa ya damu** ambayo yanahitaji mtu kuongezewa damu na kutumia dawa za matibabu maishani.

Pili, baadhi ya madaktari wanaweza kukosea **dalili za beta thalassemia** na hali nyingine na kuagiza matibabu yasio sahihi kwako.

Kujua kama una **dalili za beta thalasemia** ni rahisi.

Hatua ya kwanza ya kujua kama una **dalili za beta thalasemia** ni kumwomba daktari wako achunguze ukubwa wa seli zako nyekundu za damu. Hii inaonyeshwa na Kiasi Wastani cha Chembe za damu (MCV) cha Hesabu Kamili ya Damu yako (CBC). Heunda tayari daktari wako ana rekodi ya CBC yako kwenye faili.

Kama matokeo ya MCV yako ni 80 au chini, na HUNA upungufu wa ioni, huenda ukawa na **dalili za beta thalasemia**. Kipimo cha ziada, pamoja na hemoglobin electrophoresis, quantitative hemoglobin A2 na quantitative hemoglobin F, zitakuwa muhimu sana katika kubainisha kama una **dalili za beta thalasemia**. Vipimo hivi vinaweza kuagizwa na daktari.

Ili kuelewa jinsi thalasemia inavyoathiri mwili wa mwanadamu, lazima kwanza uelewe kidogo kuhusu damu.

Damu hubeba oksijeni kutoka kwa mapafu hadi sehemu nyingine za mwili wako. Oksijeni inabebwa na protini inayoitwa himoglobini inayopatikana ndani ya seli nyekundu za damu.

Himoglobini imeundwa na aina mbili tofauti za protini, zinzoitwa globini za alfa na beta.


Beta globini imeundwa na jeni mbili, moja inayopitishwa kwa mtoto kutoka kwa kila mzazi. Watu ambao wana jeni moja isiyo ya kawaida ya beta globini wana **dalili za beta thalassemia** (inayojulikana pia kama **beta thalasemia ndogo**).

Mtu ambaye ana **dalili za thalasemia (ndogo)** huwa amebeba dalili za jenetiki za beta thalasemia na kwa kawaida hatakuwa na matatizo yoyote ya kiafya isipokuwa upungufu mdogo wa damu,


Mara kwa mara daktari hukosea seli ndogo nyekundu za damu za mtu na **beta thalasemia ndogo** kuwa dalili za upungufu wa madini ya ioni na kuagiza virutubisho vya ioni kimakosa ambavyo havitasaidia na upungufu huo wa damu.

Ukipimwa **dalili za beta thalasemia** na upatikane kuwa na unabeba dalili hizo, mpenzi wako anastahili pia kupimwa **dalili za beta thalasemia**

ikiwa...



wazazi wote wamebeba **dalili za beta thalasemia**,



25%
upungufu wa damu
unaoitwa **Cooley**



..basi

kuna uwezekano wa **asilimia 25** kuwa **kila** ujauzito mtoto wao atarithi jeni mbili zisizo za kawaida za beta globini.

Katika hai mbaya zaidi, hii inaweza kusababisha **beta thalasemia kuu** au **upungufu wa damu unaoitwa Cooley**, tatizo mbaya sana la damu ambalo husababisha upungufu wa damu unaoitishia maisha na unaohitaji mtu kuongezewa damu mara kwa mara na huduma ya kina inayoendelea ya matibabu.

Urithi wa jeni mbili zisizo za kawaida za beta globini unaweza pia kusababisha **beta thalassemia wastani**, upungufu kiasi wa damu wenye matatizo makuu ya kiafya ikiwa ni pamoja na ulemavu wa mifupa, na kuongezeka kwa wengu.



Kwa maelezo zaidi kuhusu thalasemia, tafadhali wasiliana na: Cooley's Anemia Foundation, simu (212) 279-8090 au: info@thalassemia.org Unaweza kutembelea tovuti yetu: www.thalassemia.org

Kama wewe au mpenzi wako wote mna **dalili za beta thalasemia** na mnapanga kupata watoto, unastahili kutafuta ushauri wa mshauri wa jenetiki.